

KISWAHILI

027

15/JULAI/2026 8.30 AM-11.30 AM

MCHEPUO:

- Literature in English-French-Kinyarwanda-
Kiswahili- **(LFK)**

MUDA : Masaa matatu (3h00)

Majina:
Nambari ya usajili:

S6 DAFTARI LA MASWALI NA MAJIBU

**MTIHANI WA TAIFA 2025-2026
KIDATO CHA SITA**

MAELEKEZO:

- 1) Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
- 2) Andika majina yako na nambari yako ya usajili kwenye karatasi ya majibu kama vilivyo kwenye fomu yako ya usajili.
- 3) Mtihani huu una **maswali 22**
- 4) Mtihani huu umeundwa na sehemu kuu nne:

Sehemu ya I: Ufahamu na msamiati: Jibu maswali yote
(alama 30)

Sehemu ya II: Sarufi na matumizi ya lugha: Jibu maswali yote
(alama 30)

Sehemu ya III: Fasihi: Jibu maswali yote (alama 25)

Sehemu ya IV: Utungaji: Chagua mada moja. (alama 15)

- 5) Mwandiko wako usomeke vizuri.
- 6) Tumia kalamu ya **bluu** au **nyeusi**.
- * 7) **Tahadhari!:** Kwenye maswali ya kuchagua, weka mduara (o) kwenye herufi ya jibu lililo bora.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Maswali	Alama	Maswali	Alama
1		16	
2		17	
3		18	
4		19	
5		20	
6		21	
7		22	
8		23	
9		24	
10		25	
11		26	
12		27	
13		28	
14		29	
15		30	

ALAMA:...../100

SEHEMU YA I: UFAHAMU NA MSAMIATI (ALAMA 30)

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali yanayohusika

Hadithi fupi kuhusu urithi wa mali

Sululu kaamka leo moyo ukimtwetatweta. Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo. Anapapasapapasa alikoiweka kaptura yake usiku wa kuamkia leo. Vidole vyake vilivyorishai jasho vinakumbana na kaptura yenyewe. Imeanguka kwenye sakafu karibu na mvungu wa kitanda. Anainuka mara moja kitandani na kuivaa kaptura yenyewe, kaptura kuukuu ya kaki iliyoona miaka na mikaka, inayompwaya na yenye viraka vya kila sampuli makalioni. Apapasapo tena anakumbana na shati lake lisilokuwa na vifungo. Analivaa mara moja. Mwenyewe katika nyakati za ucheshi wake akiliita shati la marehemu George; akimaanisha Mzungu yeyote wa kule ughaibuni aliyewahi kulivaa shati hilo kabla halijarushwa kwenye mtumba wa nguo kuukuu kuja kuuzwa kwao Chenjeni kwa bei ya kutupa. Lakini leo, Sululu hana ucheshi. Leo si siku ya masihara. Leo ni siku ya kufa na kupona.

Sululu anamtazama mkewe ambaye bado amejikunja kitandani kama upinde akiforota. Analikumbuka joto alilolifaidi kwa kulala pembeni mwa mkewe huyo, mwaka huu wa tano sasa. Miaka mitano iliyobarikiwa kwa vitoto viwili ambavyo vilikuwa vimelala sakafuni kwenye kigunia kichakavu, navyo vinaforota. Miaka mitano ya kupanda na kushuka, ya raha na karaha ya kuishi na mwanamke huyu. Miaka mitano ya kupumbaa kwa hari ya kulala karibu na mwanamke huyu, joto la kiwiliwili cha mwanamke aliyejisabilia kwake na kumnyenyekea yeye kama mume anavyostahili kunyenyekewa.

Leo Sululu hana hakika kama haya yataendelea kuwa yalivyo maana leo ni siku ya siku. Leo nadhari ya Sululu imetua kwenye kero, kero ambayo chanzo chake si mwanamke huyu. La! Mwanamke huyu aliyelala pale kitandani akiforota ana kero zake vilevile, kama vile usununu usiokuwa na maana wala msingi, kudai yasiyowezekana, kumnyamazia kwa siku, majuma hata miezi. Leo linalomkaa moyoni zaidi ni kero kutoka kwa babake mzazi.

Licha ya yeye kuwa mwanamume mzima ambaye ameo, baba bado amekataa katakata kumkatia kipande cha shamba. Shamba lenyewe kubwa. Wengine huliita 'shamba maddal basari'. Kwa nini mzee huyu hataki kunipa shamba au kunipa urithi wangu? Mbona mimi ni mwanawe kindakindaki ati? Au hana hakika juu ya hilo. Sasa asiponipa shamba ndio kusema kwa nini alinizaa? Kwa nini kunileta duniani nami hilo sikuomba nifanyiwe.

Sululu akili zinamduru. Anapapasa tena karibu na kizingiti cha mlango na kupata alichokuwa anakitafuta. Vyanda vyake vinakutana na upande wa mafutuni wa panga lililojipanga vizuri mithili ya mundu. Anafungua mlango taratibu na kujitosa nje huku hamaki zimesakama, anapumua na kupuma kama mkimbiaji wa mbio za nyika mwishoni mwa mashindano. Anaelekea kwenye nyumba ya babake. Nyumba ya babake si nyumba ya kupigiwa mfano. Si jumba la Fahari.

Katika hatua ya kupunguza gharama, Mwalimu Kauka, kama alivyojulikana hata baada ya kustaafu, aliamua kutumia udongo kushikamanisha tofali na jingine. Sululu alipoitazama hiyo nyumba, aliingiwa na gere. Si nyumba ya msonge yenye kuta za mbavu za mbwa kama alimoishi yeye na familia yake changa. Kama baba angenikatia shamba, ningeacha kuchapa mtindi, niache kulewalewa, kuvaa miwani kama wengine wasemavyo, nijikalifu kulima kilimo chenye tija nipate angalao mtaji wa kujenga nyumba ya maana. Ningelima miwa, mahindi, muhogo, mtama, nyanya, njugu, ilmuradi mambo yangu yangetengenea. Ningefuga ng'ombe, farasi, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku.

Sululu alifika mlangoni kwa wazee wake na kubisha kwa hamaki.

"Fungua!"

"Nani?" Alijibu mama mtu.

"Nimesema fungua!" Aliwika Sululu.

Mlango ulifunguka muda mfupi baadaye na Sululu akauona uso wa mamake mzazi. Kwa kumwona mwanawe alivyolikamata panga na uso umepiga makunjo, mama mtu aliachama.

"Sululu kulikoni mwanangu?"

"Wapi baba?" Sululu aliuliza kwa ukali.

"Sululu!" "Nasema wapi baba?"

"Kwani kuna nini?"

"Kama baba hawezi kusikia kwa maneno sasa atasikia kwa panga."

"Mwanangu siku hizi unatuvutia bangi?"

"Kasumba au bila kasumba mimi nataka shamba!" Alifoka Sululu.

"Mnataka niseme mara ngapi? Nataka kasma yangu ya shamba."

"Sululu, umemshikia babako panga kwa ajili ya shamba?"

"Mbona hanipi fungu langu? Enh?"

"Na kwa sasa umejenga nyumba wapi?"

"Kwa shamba la baba."

"Nani kakupa ruhusa kujenga?"

"Yeye." "Sululu, umekuwa punda unashukuru kwa mateke?"

"Sasa hivi viekari viwili anavyonipa nikajenga nyumba na ninakolima kila mwaka vinanitosha nini?"

"Basi wacha kupaza sauti kama mwehu mwanangu, babako unajua tena hali yake taabani."

"Hapana, nataka shamba, nataka ekari kumi na nipewe na hatimiliki."

"Shamba hili lina ekari ishirini tu, sasa nduguzo Ayubu, Toili na Matayo watapata nini? Ehe! Wao na familia zao?"

"Sitaki kujua. Mimi ndiye mkubwa nastahiki fungu kubwa. Tena nipewe hatimiliki yenye jina langu. Iandikwe Sululu Kauka. Tena kwa herufi kubwa."

"Na isipokuwa hivyo?"

"Nitamwua mtu. Nitampasua huyu mzee tumbo lake kubwa kwa panga hili."

"Hebu sikiza Sululu," alisema mama kwa upole.

"Sisi wazazi wako tumejisabilia kwako si haba. Tumejikusuru kukupeleka shule Teremi ukakataa kusoma mwenyewe. Karo tuliyolipa ikaenda bure. Wadogo zako walitumia vyema fursa zao shuleni, sasa wana makazi ya maana."

“Sasa unanisimbulia?”

“Nasema utundu wako umezidi, mtoto husaidiki.”

“Nitamwua mtu.”

“Basi kama upo tayari kuua, anza nami hapa mamako, niliyekubeba tumboni miezi tisa, nikakuosha, nikakunyonyesha, nikakuongoa, nikakuuguza, nikakupakata...”

“Acha masimbulio!” Alipaza tena sauti.

“Ee! Wajua babako mgonjwa, usimpigie kelele namna hiyo. Amekesha akiugua.”

“Sasa anataka kufa kabla hajanipa shamba?”

“Sululu!” “Mimi nitammaliza!”

“Kizingiti hiki hupiti mwanangu. Utaniua mimi kwanza kabla kumwua babako.”

“Mama Sululu!” Sauti ya baba mtu ilisikika kutoka chumbani.

“Mwachie, aje animalize kama hiyo ni azma yake. Mwachie aje.”

Kimya kikajiri kitambo. Punde si punde Sululu aliona mlango unafunguka wazi na babake anapishwa na mama na kutoka nje. Baba alikabilia mkabala na Sululu. Mzee uso umetulia ingawa anatembea kwa kuchechea.

“Sululu!” Alimwita mwanawe kwa uanana.

“Nipe kasma yangu ya shamba.”

“Ndiyo sababu unataka kunikatakata kwa panga!” Baba alimkaribia mwanawe na kumtazama kitambo.

“Basi nipo hapa nikate vipande vipande jinsi unavyotaka.” Kimya.

“Nasema nikate kama unavyotaka shamba hili likatwe!”

“Niue mimi, umwache mume wangu,” mama alijaribu kuingilia kati.

“Sululu,” baba alitoa kauli tena.

“Hili shamba unalotaka kuniulia nimerithi kutoka kwa nani?”

“Sijui.”

“Je, kanirithisha babu yako?” Sululu alitikisa kichwa.

“Nimelinunua kwa jasho langu mwenyewe, kwa kipato kidogo cha ualimu. Kwa kudunduliza. Kwa kujihini. Kujinyima kila raha ili wanangu wawe na pahala pa kupaita pao.”

“Ninataka pangu!”

“Hutaki penu?”

“Petu si pangu.”

“Mbona usifuate nyayo zangu basi kama walivyofanya wadogo zako?”

“Sikuelewi.”

“Kwa hiyo wataka kuniua tu bila kunielewa? Hivyo ndivyo hekima yako inavyokuongoza?”

Mwalimu Kauka akauingiza mkono kwenye mfuko wake wa koti. Hapo Sululu alishtuka na kurudi kinyumenyume.

“Ala! Baba unataka kunipiga risasi?” Alilalama Sululu. Baba mtu alicheka tu.

“Tangu lini umeniona na bunduki Sululu mwanangu?”

Kisha baba akatoa bahasha na kumwambia Sululu asome stakabadhi zilizokuwa ndani. Mwanzoni Sululu alisita. Mama naye alikuwa amesimama pale anatazama sinema hiyo kwa zingatia. Hatimaye, Sululu alijipa ujasiri akamsogelea babake na kuichukua bahasha ile. Akaitoa barua ya kwanza. Ilikuwa hati ya kiapisho iliyotiwa

saini na nduguze wadogo na hakimu pamoja na kupigwa muhuri rasmi wa mahakama. Sululu alisoma kwa ghibu mara mbili mbili:

Sisi wafuatao, Toili Kauka, Ayubu Kauka na Matayo Kauka, tunathibitisha kwa saini zetu kwenye hati hii ya kiapisho mbele ya mahakama ya Chenjeni kwamba hatuna nia yoyote kudai kasma yetu kwenye ploti nambari 341 eneo la Chenjeni, shamba la baba yetu Albert Kauka. Kama baba akiona sawa anaweza kumpa ndugu yetu Sululu Kauka kasma zetu.

Ujumbe unapomtua Sululu akilini, anaingiwa na kitetemeshi na kudondokwa na machozi. Alipoichomoa hatimiliki ya kasma yake na ya ndugu zake, hatimiliki yenye jina lake, katika herufi kubwa, macho yake yalikuwa hayaoni tena kwa gharika ya machozi. Pu! Panga lake likabwagika chini bila ya habari. Siku hiyo watu wa Chenjeni walikuwa na kazi kubwa ya kumzuia Sululu kujitosa kwenye uketo wa mto Chenjeni alikotaka kujifia.

Maswali ya ufahamu wa kifungu cha habari

Tanbihi: Kuhusu maswali ya kuchagua, miongoni mwa majibu yaliyotolewa, chagua na uweke mduara (O) kwenye herufi ya jibu lililo bora.

- 1) Sababu kuu iliyomfanya Sululu aamke akiwa na hamaki ni ipi? **(alama 2)**
 - A) Ugonjwa wa baba yake.
 - B) Umaskini wa familia yake.
 - C) Kukataliwa kupewa sehemu ya shamba na baba yake.
 - D) Ugomvi na mke wake.
- 2) Sululu anamaliza muda gani akiwa na mke hadi siku ya tukio? **(alama 2)**
 - A) Miaka mitatu.
 - B) Miaka mitano.
 - C) Miaka saba.
 - D) Miaka kumi.
- 3) Sululu na mke wake wana watoto wangapi? **(alama 2)**
 - A) Watoto wawili.
 - B) Watoto watatu.
 - C) Watoto sita.
 - D) Mtoto mmoja.
- 4) Ni kitu gani Sululu alikichukua alipokuwa akielekea nyumbani kwa baba yake? **(alama 2)**
 - A) Fimbo
 - B) Jiwe
 - C) Panga
 - D) Shoka
- 5) Kwa nini baba yake Sululu hakumpa shamba mapema? **(alama 3)**
 - A) Shamba lilikuwa dogo sana.
 - B) Sululu alikuwa bado mdogo.

- C) Kulikuwa na watoto yatima waliopaswa kuzingatiwa.
D) Kulikuwa na ndugu wengine waliopaswa kuzingatiwa.
- 6) Ni jambo gani lililomfanya Sululu abadilishe msimamo wake mwishoni mwa hadithi? **(alama 3)**
A) Mama yake kumlilia.
B) Baba yake kuugua sana.
C) Kusoma hati ya kiapisho na hatimiliki.
D) Hofu ya kukamatwa na polisi.
- 7) Ndugu zake Sululu walichukua uamuzi gani kuhusu shamba? **(alama 3)**
A) Kuligawa sawa kwa wote.
B) Kumlazimisha baba kuligawa.
C) Kukataa shamba kabisa.
D) Kumpa Sululu sehemu yao.
- 8) Kauli "Petu si pangu" inaonyesha nini kuhusu tabia ya Sululu? **(alama 4)**
A) Uvumilivu
B) Ubinafsi
C) Uaminifu
D) Ujasiri
- 9) Funzo kuu la hadithi hii ni lipi? **(alama 4)**
A) Urithi hupatikana kwa nguvu
B) Watoto wategemee mali ya wazazi
C) Hasira na tamaa huleta majuto
D) Utajiri ni muhimu kuliko familia
- 10) Muhtasari wa hadithi hii ni: **(alama 5)**
A) Sululu anaondoka nyumbani kwao baada ya kugombana na mke wake kuhusu umaskini unaowakumba. Anaamua kwenda mjini kutafuta kazi ili apate pesa za kununua shamba lake mwenyewe. Mwisho wa hadithi, Sululu anafanikiwa na kuwasahau wazazi wake kabisa.
B) Sululu ana hasira kali kwa baba yake ambaye hajampa urithi wa shamba. Hali hii inayomfanya kwenda nyumbani kwa wazazi kuwadai urithi wake kwa hasira kubwa. Baba yake anamweleza kuwa shamba ni jasho lake na kwamba ndugu zake wameamua kumpa Sululu sehemu yao. Sululu anajuta sana, na anajifunza umuhimu wa subira na heshima kwa wazazi.
C) Baba yake Sululu anamnyang'anya shamba na kuligawa kwa ndugu zake wadogo pekee. Sululu anakata tamaa, anaondoka Chenjeni na kuapa kutorudi tena nyumbani. Hadithi inaonyesha madhara ya upendeleo katika familia.
D) Sululu anapigana na baba yake kwa sababu ya mgogoro wa mipaka ya shamba. Viongozi wa kijiji wanaingilia kati na kugawa shamba kwa usawa kwa wanafamilia wote. Mwisho wa hadithi unaonyesha ushindi wa haki kupitia mamlaka za kijiji.

SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 30)

- 11) Weka sentensi zifuatazo katika hali kanushi: (alama 6)
- A) Mteja akihudumiwa vizuri anafurahi.
 - B) Raia wote wamehudhuria uchaguzi mkuu.
 - C) Fanyeni haraka, tuna kazi nyingi mno.
- 12) Panga vizuri maneno ili yaunde sentensi yenye maana. (alama 4)
- A) haumei changaraweni mgomba ukipandwa.
 - B) duara ulibainisha kwamba utafiti dunia ni.
- 13) Taja aina ya kila neno lililo katika sentensi zifuatazo: (alama 4)
- A) Watoto na mama wanaimba.
 - B) Wawili walipata alama nzuri.
- 14) Andika sentensi zifuatazo katika wingi: (alama 6)
- A) Ng'ombe ndiye mnene kuliko mbuzi.
 - B) Usiende nje bila kuarifu mzazi wako.
 - C) Mtafiti ana uhuru kutoka kwa mdhamini wake.
- 15) Jaza aya ifuatayo kwa kutumia maneno uliyopewa katika mabano (). (alama 6)

(elimu, kuwahudumia, uamuzi, warithi, kujadiliwa, binafsi)

Suala ni jambo linalotakiwa na kukatiwa shauri. Suala linaweza kuwa wa serikali wa walio maskini hohehahe kwa kuwapa ng'ombe, kwa wote, haki ya wanawake kuwa na kadhalika. Ni lazima kuelewa suala ili kuweza kutoa maoni

- 16) Kwa kutumia mshale (→), husisha kipande cha sentensi kutoka **sehemu A** na kile kutoka **sehemu B**, ili kuunda sentensi yenye maana kamili. (alama 4)

Sehemu A	Sehemu B
A) Ngozi za wanyama hutumiwa	1. waharibifu
B) Farasi ana mbio	2. tunatakiwa kuheshimiana
C) Panya ni wanyama	3. kutengeneza viatu na mikoba
D) Maishani mwetu	4. kuliko ng'ombe na mbuzi

SEHEMU YA III: FASIHI (ALAMA 25)

- 17) Bainisha tamathali za usemi zilizotumiwa katika tungo zifuatazo, kwa kuzingatia maandishi yenye mwandiko mzito:

(alama 4)

- A) Alikuwa anavaa kaptura **yenye viraka vya kila sampuli** makalioni.
B) Siku hiyo, sote tulikuwa nyumbani. **Jua liliaga miti** na nuru ya mchana ikafifia.

- 18) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayohusika:

(alama 8)

Ujana

Ewe ulo na busara, fikiri bibi na bwana,
Fikiri lilo tohara, na lile lilo dhamana,
Pia fikiri izara, wewe nayo kukutana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

Ujana ni jambo bora, ameumba Rabana,
Tena umetia fora, ulitendalo hufana,
Basi usiwe mkora, akiba aweke sana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

Kuweka jambo dharura, jihimu kuweka mwana,
Siyo pato kulipura, kwa usiku na mchana,
Ukitoweka ujura, elewa umekubana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

- A) Shairi lina beti ngapi?
B) Taja kibwagizo katika shairi hili.
C) Taja kina cha kati na kina cha mwisho katika kibwagizo.
D) Taja mizani katika mshororo wa tatu.

(alama 2)

(alama 2)

(alama 2)

(alama 2)

- 19) Oanisha kila aina ya nyimbo na maana zake:

(alama 4)

Aina ya nyimbo	Maana
a) Nyimbo za mapenzi	1) Ni nyimbo za kuwasifu viongozi wa kisiasa, kuunga mkono mfumo wa utawala fulani na kuonyesha uzalendo kwa kusifia taifa au nchi
b) Nyimbo za kazi	2) Huimbwa wakati wa huzuni au simanzi, msiba, njaa,... ili kuwapa matumaini waombolezaji
c) Nyimbo za kisiasa	3) Huimbwa na mtu kwa kumsifia mpenzi wake hasa kwa tabia zake, urembo wake au mwenendo wake
A) Nyimbo za maombolezo	4) Huimbwa wakati wa kufanya kazi ili watu wasichoke. Kazi hizo ni kama vile kilimo, kusuka, uvuvi, useremala, uashi na kadhalika.

(alama 6)

- 21)** Tegua kitendawili kifuatacho:

(alama 3)

- ## SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (ALAMA 15)

(alama 15)

- A) Umoja wetu ndio nguzo yetu.
B) Vijana katika maendeleo ya nchi.

[illegible]

QUALITY CHECK



-Mwisho-